

BURAMU INSHA
KIDATO CHA TATU
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KISWAHILI KARATASI YA KWANZA 102/1

1. Swali la kwanza ni la lazima
 - ✓ Mtahiniwa atunge barua rasmi
 - ✓ Barua rasmi sharti ishughulikie mambo makuu yafuatayo.

A) Sura.

- Sura ionyeshe mambo yafuatayo.
- i. Anwani mbili – ya mtunzi
-ya mpokezi
 - ii. Tarehe ya kuandikwa kwa barua
 - iii. Mtajo – kwa mhariri
 - iv. Lengo la barua kwa mhariri
YAH:....
KUH:....
 - v. Mwili wa barua – hoja za mtahiniwa zifafanuliwe hapa kikamilifu.
 - vi. Hitimisho – mimi wako mwaminifu
-mimi wako mtiifu n.k
 - vii. Sahihi
 - viii. Jina rasmi la mwamdishi wa barua.

B) Maudhui.

Maudhui yaonyeshe sehemu mbili kuu yaani:

Visa vya utovu wa usalama

- i. Mashambulizi ya kigaidi kama vile kisa cha ‘westgate mall’ mjini Nairobi, mauaji ya walimu Mandera n.k
- ii. Visa vya wizi wa mifugo kati ya Pokoti, Turkana, Nandi, Luo, Kapedo n.k.
- iii. Wizi wa mabavu
- iv. Mauaji ya watu mashuhuri serikalini
- v. Polisi kushirikaina na wahalifu
- vi. Maandamano ya raia/wananchi yanayohatarisha amani na usalama.
- vii. Utekaji nyara wa watoto
- viii. Ubakaji.

2. Athari zinazosababishwa ba ukosefu wa usalama nchini.

- i. Kufungwa kwa shule, biashara katika maeneo hatari.
- ii. kuogofya waekezaji katika maeneno hatari basi kubaki nyuma kimaendeleo.
- iii. vifo vya watu/maafa.
- iv. Uharibifu wa miundo misingi ya nchi kama vile barabara, reli , majengo ya biashara n.k.
- v. Wataalamu kuhamia maeneo hatari na basi kusababisha uhaba wa

- huduma muhimu. Mfano matibabu, masomo.
- vi. Kutengana kwa familia
 - vii. Kupanda kwa garama ya maisha. Bidhaa mbalimbali kuongezwa bei.

1. **Tanbihi.**

Insha ikikosa sura ifaayo, mwanafunzi akadiriwe ifaavyo kisha aondolewe alama nne (4) za sura.

2. **Faida (kuunga)**

- i. Mgao sawa wa rasilimali ya nchi.
- ii. Kubuni nafasi za ajira
- iii. Kuboresha huduma za afya, kilimo n.k
- iv. Kuhushisha raia au wananchi katika maamuzi ya miradi inayowahusu katika gatuji zao.
- v. Kupeleka maendeleo hadi mashinani, mfano ujenzi wa shule, hospitali, barabara.
- vi. Kuhifadhi utamaduni chanya ya jamii za gatuji husika. Mfano Tamasha za muziki, mashindano ya urembo.
- vii. Inahimiza uwajibikaji na uzalendo(Kaunti yetu)
- viii. Huachangia ushindani chanya kati ya kaunti mbalimbali na mwishowe kuboresha maendeleo.

Hasara za ugatuzi (kupinga)

- i. Uchumi wa nchi hauewezi kustahimili mahitaji mengi ya gatuji.
- ii. Migomo ya wafanyikazi ya kila mara.
- iii. Huduma mbovu kwa umma, mfano: afya kutokana na usimamizi mbaya.
- iv. Siasa chafu – zinazochangia kudidimia kwa maendeleo, mfano kila wakati siasa za kung'atua Gavana madarakani.
- v. Huchangia ukabila- mfano ubaguzi katika ajira.
- vi. Huchangia ubinafsi na tama. Safari za kujifaidi, magari makubwa n.k
- vii. Kukwamizwa kwa maendeleo katika baadhi ya gatuji.
- viii. Mvutano kati ya serikali kuu na serikali za gatuji.

TANBIHI.

- ✓ Mtahiniwa anaweza kujadili upande mmoja kwa mfano hasara tu. Huyu anahitajika kufafanua kikamilifu angalau hoja tano (5) ili kukadiriwa vyema kimaudhui.
- ✓ wapo watakaosema moja kwa moja kuwa ugatuzi una faida tu. Hawa pia wajaadili angalau hoja tano (5) ili kukadiriwa vyema kimaudhui.
- ✓ watakaojadili pande zote mbili sharti wafafanue angalau hoja tatu (3) za kupinga na mbili za kunga au tatu (3) kuunga na mbili (2) kupinga, kisha waonyeshe msimamo wao.

3. Hii ni insha ya Methali.
 - i. Mchongoma – Mti wenye miiba

- ii. Ngoma- shida, ugumu mwingi.
- ✓ Kupanda mchongoma ni rahisi lakini kushuka chini ni vigumu.
 - ✓ Mambo mengi ni rahisi kuyatenda lakini matokeo yake huwa ya kuumiza.
 - ✓ kisa kidhihirishe maana ifuatayoo; kwamba mtu amejilingiza katika shida na sasa amekwamia humo na hawezi kujitoa ndani tena.

Tanbihi.

- ✓ Vipengele vitatu vijitokeze: Utangulizi, mwili, hitimisho.
 - ✓ Kichwa cha makala kidhihirike
 - ✓ Sharti insha idhihirishe jinsi ambavyo mhusika alijiingiza katika tatizo/shida fulani na mwishowe akashindwa kujitoa ndani.
 - ✓ Atakaye jihusisha au ahusishe mtu mwingine atakuwa amejibu swali.
 - ✓ Mtahiniwa ashughulikie pande zote mbili za methali. atakayeshughulikia upande mmoja asipite alama 10. (c+)
4. Hii ni Insha ya kubuni
- ✓ Mtahiniwa atunge kisa ambacho kinaoana na mwisho huu.
 - ✓ Insha ya mwanafunzi ionyeshe tukio/kisa cha kuogofya kama vile, ujambazi, uporaji wa mali, vita vya kikabila, uvamizi wa uhalifu, mkasa wa moto n.k.
 - ✓ Kisa kitungwe na kusimuliwa katika nafsi ya kwanza umoja, katika wakati uliopita

Tanbihi.

- ✓ Lazima mtahiniwa amalizie kwa maneno aliyopewa.
- ✓ Anayepunguza au kuongeza maneno hadi manne ya kimalizio aondelewe maki mbili (2) za dondoo.